

# Anayeafikiana Na Imamiyya Katika Baadhi Ya Nukta

Pia wapo wanaoafikiana na Imamiyya katika baadhi ya nukta za suala hili.

An-Nawawy amenukuu kwa kusema: Atwau na Tausi wamesema: “Kivuli cha kitu kikilingana na kitu chenyewe hapo umeingia wakati wa Al-Asr na ufuatao ni wakati wa Adhuhuri na Al-Asr kwa kushirikiana mpaka jua litakapozama.

Kauli hii inahusu Adhuhuri kwa kivuli cha kitu kulingana na kitu husika, kisha inafanya wakati uliobaki ni wa kushirikiana Adhuhuri na Al-Asr mpaka jua litakapozama. Kauli hii inakaribiana na ile ya Imamiyya.

Malik amesema: “Kivuli kikilingana na kipimo cha kitu kilichosimama ndio mwisho wa wakati wa Adhuhuri na mwanzo wa wakati wa Al-Asr kwa kushirikiana. Hivyo kivuli kikizidi kipimo ziada ya wazi basi wakati wa Adhuhuri umekwisha.<sup>1</sup>

Kauli hii inafanya sehemu ya wakati kuwa wakati wa kushirikiana kati ya Adhuhuri na Al-Asr nao ni – baada ya kivuli kulingana na kipimo cha kitu kilichosimama – mpaka kivuli kinapokizidi kipimo hicho kwa ziada ya wazi, ni wakati wa kushirikiana kati ya Adhuhuri na Al-Asr.

Pia imenukuliwa toka kwake kuwa, wakati wa Adhuhuri unaendelea mpaka kuzama kwa jua.<sup>2</sup>

Na kuna kauli nyingine ambazo zina namna fulani ya muafaka na fiqhi ya Imamiyya.

---

1. Al-Majmuu, Juz. 3, Uk. 24

2. Al-Majmuu, Juz. 3, Uk. 27

---

## Source URL:

<https://www.al-islam.org/sw/kukusanya-sala-mbili/anayeafikiana-na-imamiyya-katika-baadhi-ya-nukta>